

SEHEMU YA SABA
UHALALI WA SHUGHULI

63.-(1) Kiwango cha mikutano na vikao vyote vya Bunge wakati wa kufanya maamuzi kitakuwa ni nusu ya Wabunge wote.

Kiwango
cha
Mikutano

(2) Mara kabla ya uamuzi wowote kufanyika ikiwa Mbunge yeyote aliyehudhuria atapinga kwa kudai kwamba, mbali na Spika au, endapo Spika hayuko kwenye Kiti basi Naibu Spika au Mwenyekiti wa Bunge, Wabunge waliopo ni chini ya nusu ya Wabunge wote, basi kama Spika au Naibu Spika au Mwenyekiti wa Bunge atatosheka kuwa hali ya mambo kweli ndivyo ilivyo; atasimamisha shughuli kwa muda wa dakika tatu na huku Katibu akipiga kengele kwa vituo yaani siyo mfululizo.

(3) Endapo shughuli zimesimamishwa kwa mujibu wa fasili ya (2), basi wakati wa Bunge kurudia shughuli baada ya wakati uliotajwa kwisha, Spika, Naibu Spika, au Mwenyekiti wa Bunge atahakikisha kama idadi ya Wabunge waliopo bado imepungua nusu ya Wabunge wote, na kama muda mfupi zaidi, kama atakavyoona inafaa.

Nafasi
wazi
Bungeni

64. Bunge halitahararnishwa kufanya shughuli zake kwa sababu tu ya nafasi yoyote ya Mbunge kuwa wazi.

Kupiga
Kura
Bungeni

65.-(1) Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 46A na 98 za Katiba, mambo yote yanayohitaji kuamuliwa na Bunge yataamuliwa kufuata maoni ya Wabunge walio wengi waliohudhuria na kupiga kura Bungeni.

(2) Spika, Naibu Spika, na Mwenyekiti wa Bunge, wakati anapokuwa amekalia kiti cha Spika, hatakuwa na, kura ya kawaida bali atakuwa na kura ya uamuzi, endapo kura za "ndiyo" na "siyo" zitalingana

(3) Wakati mjadala juu ya hoja fulani unapomalizika, Spika atawahoji Wabunge ili kupata uamuzi wao juu ya hoja hiyo kama ilivyokuwa au baada ya kufanyiwa mabadiliko, Spika kwanza atataka uamuzi wa wale wanaoafiki kwa kusema " Wale wanaoafiki waseme "Ndiyo" Kisha atataka uamuzi wa wale wasioafiki kwa kusema "Wale wasioafiki waseme "Siyo".

(4) Isipokuwa kama imeelekezwa vinginevyo katika Kanuni hizi, uamuzi juu ya mambo yote utapatikana kwa kufuata uwingi wa sauti za Wabunge za kusema "Ndiyo" au "Siyo" na Spika atatangaza matokeo ya kura kwa kusema "Nafikiri walioafiki wameshinda" au "nafikiri wasioafiki wameshinda". Baada ya kusema hivyo, Spika ataruhusu muda upite ili kutoa nafasi kuhakikisha, uamuzi wa Bunge juu ya jambo hilo; na katika muda huo Mbunge yeyote aweza kusimama mahali pake na kusema "Kura zihesabiwe" Endapo hakuna Mbunge aliyedai hivyo, Spika atatoa kauli ya uamuzi wa mwisho kwa kusema; "Walioafiki wameshinda" au "Wasioafiki wameshinda"vyovyote itakavyokuwa.

(5) Iwapo Mbunge yeyote atadai kura zihesabiwe, basi Spika ataamuru kura. zihesabiwe ikiwa:-

- (a) anafikiri kwamba kuna shaka ya kutosha juu ya matokeo ya kura hiyo, au
- (b) Wabunge wengine kumi au zaidi watasimama mara moja mahali pao wakiunga mkono dai la kura kuhesabiwa.

(6) Endapo Spika ataamuru kura zihesabiwe, Katibu atapiga kengele ya kahesabu kura kwa muda wa dakika moja, na baada ya muda huo Katibu ataanza kuchukua kura, kwa kuita Mbunge mmoja mmoja kwa jina lake na kumwuliza anapiga kura yake upande gani, na kuiandika kura hiyo ipasavyo

Kisha katibu atatangaza idadi ya wale wanaoafiki, wasioafiki na wasiokuwa upande wowote; na Spika atatangaza rasmi matokeo ya hesabu hiyo ya kura

(7) Kura zinapohesabiwa, orodha kamili itatengenezwa inayoonyesha namna kura zilivyopigwa na itaingizwa katika Taarifa Rasmi kwa ajili ya kuweka kumbukumbu rasmi ya uamuzi wa Bunge.